# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.


Sheria za majimbo **fulani** zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu **vituo ya ukaguzi** na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## HAKI ZANGU NI GANI?



- Uko na haki ya kutojishitaki weye peke. Hii ina maanisha kama uko na haki ya kubakiya kimya wakati unaulizwa maswali na polisi ao maafisa bengine ba sheria. Unaweza kusema: "Sipendi kujibiya maswali yenu."
- Uko na haki ya kutatuliwa kwa kesi yako kwa haki na bila upendeleo. Lomba ukuwe na mutafsiri kama Kingereza haiko luga yenye unajisikia muzuri zaidi kuongea.
  - Haupashwi saini kitu ata moya yenye hauelewe.
- Uko na haki zidi ya upekuzi na kufungiwa yenye haiko halali. Haupashwi kufungula mulango kusudi polisi iingiye mu nyumba yako kwa ajili ya upekuzi isipokuwa kama bako na kibali ya upekuzi ya kisheria. :
- Kama hauyafungiwa, uliza kama unafungiwa. Kama jibu ni hapana, uliza: "Je, niko huru kuenda?" Kama jibu ni ndiyo, enda kwa utulivu.
- Kama unafungiwa na maafisa wa uhamiaji, uko na haki ya kutafuta mwanasheria, lakini serikali haina haja ya kukupatiya mwanasheria -lomba mwanasheria mara moya.



- Kama unafungiwa na polisi kwa sababu ya uhalifu, uko na haki ya kupata mwanasheria wa bure (mwanasheria wa serikali) wakati ya kuulizwa maswali.
- Uko na haki ya kuwasiliana na ubalozi ya inchi yako. Maafisa wa uhamiaji na polisi banapashwa kuruhusu ubalozi wa inchi yako kukutembelea ao kuzungumuza na weye.
- Uko na haki ya kukatala rufaa zidi ya amri ya kufukuzwa mu inchi, hukumu ya uhalifu, ao kukataliwa ya ombi yako ya uhamiaji (kwa mufano, kukatala ombi ya fasi ya makimbiliyo).
- Polisi ao maafisa wa uhamiaji habapashwi kukulomba pesa kamwe.

# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

## MAMBO YENYE INAKUPASA UFANYE



- Tulia.
- Usikimbiye, usibishane, usipinge, wala usiwazuwiye polisi ao maafisa wa uhamiaji kuifanya kazi yao, hata kama unaamini haki zako zimevunjwa.
- Usiseme kitu kwa polisi ao kwa maafisa wa uhamiaji.
- Tiya mikono yako fasi kwenye polisi ao maafisa wa uhamiaji banaweza iona.
- Usiseme bongo kuhusu hali yako ya uhamiaji wala usipane hati za bongo.
- Kama uko na miaka 18 ao zaidi, kumbuka kubeba nakala ya hati zako za hali ya uhamiaji.
  - Weka nakala mu simu yako kila wakati.
  - Afisa akikuuliza kuhusu hali yako ya uhamiaji, uko na haki ya kubakiya kimya na unasema: "Sipendi kujibiya maswali yenu. Minapenda nizungumuze na mwanasheria."
- Weka mu kichwa namba ya simu ya rafiki, mwanamemba wa jamaa ao mwanasheria mwenye unaweza ita kama unafungiwa.
- Panga ni nani mwenye atalea watoto wako ao wapendwa wako wengine kama unafungiwa.
- Tayarisha batu benye bako chini ya malezi yako (kwa mufano watoto na bazazi bazee) kuhusu yenye banaweza fanya kama unafungiwa.
- Chagula mutu mwenye unaamini akufanyie maamuzi ya kipesa na kuhusu malezi ya watoto wakati hauna uwezo ya kuifanya weye peke.
- Weka hati zako za uhamiaji, rekodi za makosa ya uhalifu na hati zingine za muhimu fasi salama kwenye mutu mwenye unaamini anaweza kuzifika ako.
- Hakikisha wapendwa wako wanajua namba yako ya uhamiaji (A-Numba) na gisi ya kukupata kama unafungiwa na ICE.
- Kumbuka mambo yenye ilitokea wakati wa ile tukio, na kama inawezekana, ikamate video.
- Fikisha malalamiko kwa kuandika kama unasikiya sawa vile haki zako zimevunjwa.